

Kimeandikwa na: Edward Hughes

Kimeorodheshwa na: M. Maillot; Lazarus

Imerekebishwa na: M.Kerr; Sarah S; Alastair
Paterson

Kimetafsiriwa na: Grace Chepkoech

Kimedhibitishwa na: Bible for Children
www.M1914.org

©2021 Bible for Children, Inc.

License: Kuna ruhusa ya kuchapa hadithi hii, lakini bila ya kuuza.



Mungu amewahi kuwapa
mtoto katika familia
yako? Ni furaha
kubwa, sivyo! Isaka
na Rebeka lazima
walifurahia sana.
Mungu aliwapa
mapacha.



Watoto wale
walishindana wakiwa
tumboni mwa Rebeka.
Alipoomba, Mungu
akasema kuwa
wana wake wawili
wangeongoza
mataifa- na
yule aliyezaliwa
wa pili angekuwa
mkuu kuliko yule
mkubwa. Kawaida
mwana wa kwanza ndiye
huwa mkuu. Mwishowe
watoto wakazaliwa.



Mapacha wale hawakufanana. Esau, mwana wa kwanza, alikuwa na nywele mwilini na akawa mwindaji hodari. Yakobo alikuwa na ngozi nyororo na alipenda kufanya kazi nyumbani. Baba yao Isaka alimpenda Esau zaidi. Mama yao alimpenda Yakobo.




Siku moja, Esau alikuwa na njaa. "Nipee chakula," alimwambia Yakobo. "Niuzie kwanza haki yako ya mzaliwa wa kwanza," Yakobo akamwambia. Esau hakujali ahadi ya Mungu kwa mzaliwa wa kwanza.

Akamwuzia Yakobo haki yake. Sasa Yakobo ndiye angekuwa kichwa cha jamii baba yao atakapokufa.



Mungu akazungumzia Isaka usiku mmoja. "Mimi ndiye Mungu wa Babako, Ibrahimu. Niko pamoja nawe. Nitabariki kizazi chako." Hata kama Isaka alimwabudu Mungu, mwana wake Esau aliwaoa wanawake wawili wahiti, watu ambao hawakumwabudu Mungu.



Isaka akazeeka sana. "Tafadhali niletee nyama nzuri," akamwambia Esau. "Halafu nitakubariki." Hii ilikuwa baraka ya kipekee kutoka kwa baba kwa mzaliwa wa kwanza. Esau akaharakisha kwenda kuwinda mnyama. Lakini Rebeka alikuwa amesikia. Yeye alitaka Yakobo abarikiwe.





Rebeka akapanga njama. Alipopika chakula ambacho Isaka alipenda, Yakobo alienda kuvaa mavazi ya Esau na akaweka nywele za wanyama mikononi na shingoni mwake. Macho ya Isaka hayakuwa yanaona vyema. Sasa walitaka kumdanganya.



Yakobo akamletea Isaka chakula. "Unazungumza kama Yakobo," Isaka akasema, "lakini mikono yako ni kama ya Esau." Baada ya kula, Isaka alimbariki mwana wake aliyekuwa amepiga magoti mbele yake.



Baada ya Yakobo kuondoka, Esau akamjia Isaka.
"Ndiyo hii chakula chako baba," akasema. Hapo


Isaka akajua kuwa alidanganywa. "Siwezi nikabadilisha baraka," akalia. Moyo wa Esau ukajaa chuki kwa Yakobo. Akajaribu kumwua.



Rebeka akasikia maneno ya Esau. "Nenda nyumbani mwa mjomba wako," akamwambia Yakobo, "hadi ndugu yako atakaposahau uliyoyafanya." Isaka akakubali na pia akamwelezea atafute mke katika familia ya mamake. Sasa Yakobo akaondoka nyumbani.




Usiku huo, Yakobo
akasimama safarini
kulala, pale akatwaa
jiwe chini ya kichwa
chake. Pengine
alikuwa na upweke,
pengine aliogopa.
Lakini hakuwa peke
yake. Mungu
alizungumza



naye
katika
ndoto ya
kupendeza.





"MIMI NDIYE MUNGU WA
BABA ZAKO, IBRAHIMU
NA ISAKA. NI KO
PAMOJA NA WE.

NITAKUPA NCHI HII. KUPITIA FAMILIA
YAKO FAMILIA ZOTE DUNIANI
ZITABARIKIWA." Baada ya Mungu kuzungumza,
Yakobo akaamka. Alikuwa na hofu.



Mjomba wa Yakobo, Labani alimkaribisha. Yakobo akaja kumpenda Raheli binti Labani na akamtumikia Labani miaka saba ili apate kumwoa.



Lakini usiku wa harusi, Labani akamdanganya Yakobo.



"Huyu ni Lea, sio Raheli," Yakobo akanung'unika.
"Ulinidanganya." "Binti mkubwa ni lazima aolewe wa
kwanza." Labani akasema. "Sasa mwoe Raheli pia,
lakini unitumikie miaka mingine saba."
Yakobo akakubali. Pengine alikumbuka
udanganyifu wake kwa Isaka na Esau.



Yakobo alipata wana kumi
na mmoja. Miaka ilipopita
akatamani kuwapeleka
familia yake Kanani. Wazazi
wake bado walikuwa pale.
Lakini Esau alikuwa amesema
kuwa atamwua. Je, kulikuwa
na usalama?



Siku moja Mungu
akamwambia arudi.
Yakobo akakusanya
familia yake na
wanyama na
wakaelekea
nyumbani.



Ilikuwa safari ya ajabu. Esau akaja kuonana naye yakobo pamoja na watu mia nne. Lakini hakumwumiza Yakobo! Alimkimbilia na kumkumbatia Yakobo. Yakobo na Esau wakawa marafiki tena, na Yakobo akafika nyumbani salama.



Yakobo Mdanganyifu

Hadithi kutoka kwa Neno la Mungu, Bibilia,

inapatikana katika

Mwanzo 25-33

"Kufafanusha maneno yako kwatia nuru."

Zaburi 119:130



Mwisho



Hii hadithi ya bibilia inatueleza kumhusu Mungu wetu wa ajabu aliyetuumba na anayetaka tumjue.

Mungu anajua tumetenda mambo mabaya, anayoyaita dhambi. Adhabu ya dhambi ni mauti, lakini Mungu anakupenda sana hata akamtuma mwana wake wa pekee, Yesu, Ili afe msalabani na aadhibiwe kwa dhambi yako. Alafu Yesu akafufuka na kuenda nyumbani mbinguni! Ukimwamini Yesu na kumwomba msamaha kwa dhambi yako, Atakusamehe! Yesu atkuja na kuishi ndani yako, na utaishi naye milele.

Kama unaamini huu ni ukweli, Sema haya kwa Mungu: Mpendwa Yesu, ninaamini kuwa wewe ni Mungu, na ulifanyika mtu ili ufe kwa ajili ya dhambi zangu, ili niwe na maisha mapya, na siku moja nitaenda kuwa nawe millele. Nisaidie nikutii na niishi kwa ajili yako kama mtoto wako. Amina.

Soma bibilia na uzungumze na Mungu kila siku! Yohana 3:16

